# Ripoti ya Kongamano la Lugha, Babati – Julai 2018




## Washiriki

| Wagorwaa | Waasimjeeg | Waisanzu | Wahadzabe | Wazungu |
|---|---|---|---|---|
| Pascali Bu'ú | Mayco Bacheng | Nicholas Nalingigwa Gideon | Maria | Andrew Harvey |
| Stephano Edward | Yohani Mangi | Petro Malindeu | Gudo | Robert Lindfield |
| Mch. Hezekiah Kodi | Yonah Ndege | | Sigwazi | Richard Griscom |
| Raheli Lawi | | | | |
| Festo Massani | | | | |

Griscom, Richard, Andrew Harvey, and R. Lindfield. 2018. Report of Language Endangerment Workshop: Babati - July 2018 / Ripoti ya Kongamano la Lugha: Babati - Julai 2018. DOI: 10.5281/zenodo.2529349

## Utangulizi

Mwezi wa Julai tarehe 16 na 17, 2018, wawakilishi kutoka makundi ya makabila manne kutoka katikati ya Tanzania walikutana Babati kujadili mabadiliko wanayokutana nayo siku hizi katika jamii zao na madhara yake katika lugha yao na utamaduni, vile vile na fursa za kupambana na mabadiliko yaliyo hasi. Makundi yaliyowakilishwa ni Waasimjeeg Datoga, Wagorwaa, Wahadzabe, na Wanyihanzu. Wagorwaa na Wanyihanzu walialikwa na Andrew Harvey, mtafiti aliyekuwa akifanya kazi ya kuhifadhi kumbukumbu ya lugha hizi. Waasimjeeg Datooga na Wahadzabe walialikwa na Richard Griscom, mtaalamu anayefanya kazi kaskazini mwa Tanzania na vikundi hivi viwili, kimsingi akitumia muda wake kuhifadhi kumbukumbu za Waasimjeeg Datooga. Makundi maawili yaani Wagorwaa na Waasimjeeg Datooga wana uzoefu kufanya utafiti wao wenyewe na Wanyihanzu na Wahadzabe wanajiandaa ambapo wataanza kufanya utafiti wao wenyewe.

Malengo ya msingi ya kongamano ni kushirikishana uzoefu wa mabadiliko ya utamaduni, kuanzisha mtandao kati ya jamii tofauti zinazojihusisha katika utafiti wa lugha, kubadilishana maarifa na mafunzo kutoka miradi tofauti, na kujadili chaguzi mbalimbali kwa ajili ya uhusishaji unaowezekana na uhifadhi.

Siku ya kwanza ilitumika kujadili mada zilizoorodheshwa hapo chini, zilizoandaliwa ili kwamba vikundi vidogo vilivyogawanywa katika jamii tofauti ya lugha waweze kujadili uzoefu wao kwa kina katika maeneo yao.  Kila kikundi kilipewa nafasi ya kuwasilisha yaliyotokana na mjadala wao katika kundi kubwa, kisha mambo yanayofanana yaliyonukuliwa na wataalamu wa lugha na yalijadiliwa kwa wazi na kundi kubwa kwa uwazi na kwa pamoja. Wakati wa mjadala huu wa wazi, kila mmoja alikuwa na nafasi ya kuongea aliyonayo, na mfumo jumuishi ulitumika kumpata mwenye hoja ya kuwasilisha. Siku ya pili zoezi lilifanyika karibu na ziwa Babati, kushirikishana maarifa ya kufanya utafiti kwa wahusika. Mijadala hii ilijikita zaidi kwenye maarifa ya vitendo kama nyenzo, mbinu za kuweka kumbukumbu, na kuhifadhi taarifa.

## Maswali

*Ni mabadiliko gani ya utammaduni katika jamii unayoona leo? Unayachukuliaje?  Je unadhani kwamba mabadiliko haya ni hasi au chanya?*

Kila kikundi peke yake kilitambua kwamba lugha yao ina tatizo katika kuridhisha lugha yao kwa kizazi kinachoibukia . Wote walieleza kwamba Kiswahili kinachukua nafasi badala ya lugha zao karibu katika kila eneo: elimu, utamaduni (muziki na simulizi), biashara na maisha ya kijamii. Waisanzu walisema kwamba kila anayeongea  Kinyihanzu anaonekana kama hajaelimika na ni mjinga, mtazamo huu umefikia mpaka vijijini ambapo kuna jamii kubwa ya Waisanzu.

Vile vile, kila kikundi kilisema kuwa namna ya maisha ya kitamaduni kwa namna au nyingine yamepotea. Kwa mfano Wahadzabe walisema watoto hawajui nyimbo za

kitamaduni, Waasimjeeg Datooga walisema nyumba za kitamaduni na hata vyakula vimepotea, jambo ambalo limesababisha tatizo la afya katika jamii. Wagorwaa pia walisema kuwa imeonekana kuwa ni aibu kukiongea Kigorwaa kwa sababu ya mtazamo hasi hata kwenye jamii yenyewe. Pia walisema kwamba mbinu za elimu ya jadi imepotea, ikiwa ni pamoja na sherehe muhimu inayohusiana na nyakati za kilimo kwa mwaka mzima, ambazo ni sehemu ya urithirishaji wa lugha. Pia walihusisha matatizo ya sasa kama mimba zisizotarajiwa kama chanzo cha kupotea mfumo huu.

Mwakilishi mmoja wa Isanzu alisema makundi madogo kama Isanzu "yanamezwa" na makundi makubwa. Alitoa mfano kwamba nyimbo, michezo, na misemo mifupi yaliyotumika kuwatofautisha na makundi mengine yote imesahhaulika. Matokeo yake makundi yenye uhusiano wa karibu zaidi yanazidi kuchanganyika na kuwa mmoja. Pia waliibua hisia kwamba mfumo wa elimu ya jadi, uliowategemea wazee kufundisha vijana, umepotea.

*Nini vyanzo vya mabadiliko haya?*

Maudhui ya jumla yaliyojitokeza kwa vikundi vyote ni kwamba taratibu za jadi za kuelimisha vijana zimepotea na nafasi kuchukuliwa na mfumo wa elimu unaotumiwa na serikali. Ilisemwa kwa kurudiwa rudiwa kwamba siyo tu kwamba vijana wanafundishwa kwamba Kiswahili ni lugha ya maendeleo na biashara, bali wale wanafunzi wanaadhibiwa vikali kwa kutumia lugha zao za nyumbani jambo ambalo linaharibu mtazamo wao juu ya lugha na uwezo wao wa kukiongea. Kama ilivyotajwa hapo juu elimu rika imepotea kwa sehemu kubwa. Wagorowa kuwa hii iliambatana na kupotea kwa heshima kwa wazee na kushuka kwa mamlaka yao. Walisema kwamba wazee (pamoja na mbinu zao za kufundishia na lugha) mara zote wameonekana kama wamepitwa na wakati na kwamba hawafai. Mshiriki mmoja wa Waasimjeeg Datooga alishauri kwamba kutowaheshimu wazee na mila zao kwa sehemu inatokana na kushindwa kwao kuwa na fedha katika mfumo wa uchumi wa sasa.

Wanyihanzu walieleza kuwa ni vigumu kwa wazazi wa siku za leo kutimiza mahitaji ya watoto wao na kupata muda wa kuwaelimisha watoto wao elimu ya utamaduni wao. Walipoulizwa kwamba kwa nini watu wana shughuli nyingi kiasi cha kukosa muda wa shughuli za kitamaduni, mmoja wa Nyihanzu alijibu kwamba siku hizi kuna msukumo mkubwa wa maendeleo ya kiuchumi, hasa kumwezesha mtoto kupata elimu ya kimagharibi. Hili linalazimisha uanzishwaji wa biashara ambayo hulazimisha matumizi ya Kiswahili kama lugha ya msingi ya mawasiliano. Mshiriki wa kigorowa jinsi ambavyo wale wanaojihusisha na shughuli za kitamaduni walivyo nyuma kwani kuna mafanikio kidogo sana au hakuna kwa kujihusisha na shughuli hizo. Misamiati na fursa zinazoambatana na lugha zimepotea kabisa. Mshiriki mmoja wa Hadzabe aliongeza kuwa hata watu ambao wanahamasika kutunza utamaduni mara huwa wamechoka kutokana na shughuli za kila siku na kujihusisha na shughuli zingine.

Hadzabe na Waasimjeeg Datooga wote wawili walisema kuwa mazingira ya kiuchumi yamewalazimisha kuzungumza lugha ya makundi mengine makubwa kwenye maeneo yao kutoka na makundi yao kuwa madogo. Walisema kwamba vijana wenye elimu wanaomaliza shule huwa wanahamia mijini mahali penye fursa kubwa. Pia wote wawili walisema makundi haya makubwa huwanyanyapaa na kuwabagua jambo ambalo linawafanya vijana kujitenga mbali na asili yao. Kwa kuongezea, kila kikundi kilitaja kuwa mchanganyiko mijini na ndoa za mchanganyiko imesababisha kudhoofisha hadhi ya lugha kwa kuwa Kiswahili kinachukuliwa kuwa lugha ya mawasiliano kwa jamii zote. Sababu nyingine iliyotolewa na Waasimjeeg Datooga ambayo pia ilikubaliwa na makundi yote ni kwamba utamaduni maarufu kwa Tanzania ya leo unatawaliwa na Kiswahili na simulizi zake miongoni mwa vijana katika muziki na filamu.

*Nini ni tatuzi-akiba kwa matatizo haya?*

Mkundi yote yalikaza umuhimu wa kuhamasisha matumizi ya lugha nyumbani. Mbinu mojawapo ya kutimiza hili ni kufundisha vijana michezo na ngoma. Hili linaweza kufanyika kupitia mikusanyiko maalumu ya jamii ambapo wazee wanaweza kutoa mafundisho au kuhamasisha wazazi na wakongwe katika nyumba zao kuchukua hatua halisi kiutendaji kufundisha nyimbo za kitamaduni pamoja na michezo. Kila kikundi kilishauri kuwa wazee wa mila waombwe kuja kuwafundisha vijana hawa. Gorwaa walipendekeza kuwa wanafikiria kutumia vyombo vya habari, kama vile vituo vya redio ambavyo vitatangaza lugha ya Gorwaa na kutoa fursa kwa wanaotumia Kiswahili. Pia walishauri Kigorwa kitumike kwenye mikutano ya jamii na mikusanyiko ya kidini, wazo lililoungwa mkono na vikundi vingine. Kuhusu mada ya vyombo vya habari vinavyohusika na lugha, Waasimjeeg Datooga walishauri kuwepo kwa app yenye kumbukumbu za nyimbo na hadithi ambayo inaweza kutumiwa na jamii iliyotawanyika kukuza ujuzi wao wa lugha.

Wazo jipya la sasa ni kwamba kila jamii ina nafasi ambapo watu wanaweza kuja kusikiliza lugha yao ikitumika na kuchukua nafasi na kushiriki shughuli zao za kitamaduni. Ihanzu tayari wameanza kuweka mpango kwa ajili ya mradi huo na wametenga eneo, Wagorwaa walisema wanajadiliana kuona uwezekano wa kuwa kituo cha kitamaduni. Katika eneo hilo, matukio yanaweza kufanyika kama vile, kazi za muziki, masimulizi, mafunzo ya lugha, na yote haya yanaweza kuwafanya watu wahamasike kuhusu urithi wao na kuwapatia fursa katika kushiriki na kuhifadhi utamaduni wao. Wagorwaa waliongeza kuwa wanategemea kuwa na shamba ambapo mbinu za kilimo za jadi zitatumika, ambayo hatimaye watu watajifunza misamiati na matendo yanahusiana na kilimo, pamoja na kushika sherehe na sikukuu za kitamaduni. Wahadzabe walielezea jinsi wanavyofanya matukio hayo mara kwa mara katika jamii wakihusisha mashindano mbalimbali na michezo ya kitamaduni, ambapo matumizi ya lugha ya Hadzabe inahamasishwa. Walisema haya yamefanikiwa kuleta mafanikio makubwa katika kuileta jamii pamoja na kuwafanya watu kuongea Kihadzabe.

Waasimjeeg Datooga na Wagorwaa walikaza kwamba wamejisikia kuwa sehemu ya suluhisho ni kuwa na mambo yaliyowekwa katika maandishi katika lugha zao ambazo zitatumika kuelimisha vijana na kuhifadhi maarifa kwa lugha zao. Walisikia kuwa ikiwa watu wataweza kutumia lugha yao katika maandishi kuwasaidia kuona kuwa lugha yao ni muhimu na kuwapa motisha vijana kujithamini lugha yao. Katika kuongezea kwenye hili, mshiriki mmoja wa Hadza alishauri kuwa taarifa hii itafsiriwe na kusambazwa kwa watu kwenye jamii mbalimbali, wakitumaini kupata mtazamo wa changamoto zinazowakabili kuhusu utunzaji wa utamaduni na lugha ili kuwahamasisha watu kutafuta suluhisho.

Mshiriki mmoja wa kundi la Hadzabe alisema kwamba, alijisikia kuwa chanzo kikubwa cha tatizo ni ardhi. Alitoa maoni kuwa mengi ya matatizo yamesababishwa na ukosefu wa ardhi ya mababu, na kuwabana na kushindwa kuishi kwa kufuata mbinu za jadi kuwinda na mwendelezo. Kwa hiyo, alisema kuwa ikiwa haki ya umiliki wa ardhi ingeboreshwa kwa Wahadzabe, mengi ya matatizo haya yatapata suluhisho. Kwa mfano, hawatahitaji tena kuwavutia watalii kama chanzo cha mapato au kutafuta kazi katika jamii za jirani.

*Tunawezaje kufanya kazi kwa pamoja katika makundi haya tukishirikiana na wataalamu wa lugha kufikia utatuzi/malengo?*

Swali lililenga kutoa fursa kwa baadhi ya tafakuri kwa hatua zinazofuata kwa wote wawili waandaaji na washiriki. Kulikuwa na hisia kali sana ya kutaka kuendelea kufanya kwa pamoja ili kushughulika na baadhi ya mambo yanayokabili jamii mbalimbali. Pendekezo moja ni kwamba jamii nyingine zitembelee Wahadzabe wakati wa mashindano yaliyotajwa hapo juu kuona yanavyotumika kutoa nafasi kwa ajili ya utamaduni na matumizi ya lugha ya Kihadzabe. Wote tulipeana mawasiliano ili kushikamana na kutumaini kuwa na mtandao kati ya jamii hizi na kushirikishana habari na kuweza kuwa na rasilimali nyingi.

## Tafakuri na Hitimisho

Kwa ujumla, mkutano huu ulifanikiwa sana kwa kuanzisha mazungumzo ya kuwa na ushirikiano kati ya jamii hizi, ambayo tunaamini itasababisha mjadala na ushirikiano siku za usoni. Tuliweza kupata taswira ndogo ya madhara ya mabadiliko ya lugha na utamaduni katika eneo la Kaskazini mwa Tanzania na nini ni msukumo wa mabadiliko hayo. Mkutano ulikuwa wa kirafiki na wa kufurahisha, na ulileta ufahamu wa jamii mbalimbali na changamoto zinazowakabili, ambazo zilikuwa zilituelimisha kwa kiwango sana kibinafsi.

Ilituwia vigumu kugusa hata kwa juu juu katika mjadala wa hatua zipi zichukuliwe katika juhudi ya kupunguza matokeo hasi ya mabadilliko haya, lakini tulianza kusikia maono na matamanio ya jamii mbalimbali kuhusu mpango utakavyoonekana. Kwa kutafakari, ingekuwa ni muhimu kuwa na mtu mwenye uzoefu wa miradi ya uhuishaji wa lugha ambayo angetupa mifano inayofaa. Ikiwa mkutano kama huo utatokea tena, hili ni muhimu likazingatiwa.

Jambo moja zaidi ni kwamba mkutano ulikuwa umetawaliwa na wanaume, wanawake walikuwa ni wawili tu. Kwa kuendelea mbele ni muhimu kuwa na uwakilishi sawa ili kuwapa wanawake sauti na kuwa maoni tofauti na uzoefu kutoka tamaduni na jamii mbalimbali.

Ahsante kwa kusoma na ninatoa shukrani nyingi kwa kila mmoja aliyehudhuria kwenye mkutano. Isingewezekana bila muda wenu, shauku yenu na maono.